

شَفَاعَةُ الرَّحْمَنِ
وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آتَيْنَا مِنْكُمْ وَمَكَلِّفُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْسَخْنَا
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ لِئَلَّا أَنْقَضُنَا لَهُمْ وَلَمْ يَجِدُنَا لَهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهُمْ أَثْنَانًا
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



Toleo: 1446 / 02

Ijumaa, 26 Safar 1446 H

30/08/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Miradi Mikubwa katika Nchi Changa Haipo Kuhudumia Raia

(Imetafsiriwa)

Majibu ya karibuni ya serikali Bungeni kuititia Naibu Waziri wa Nishati Judith Kapinga kuhusiana na kupunguza gharama za umeme kwa sababu ya kuanza uzalishaji umeme katika Bwawa la Kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) ni kauli ya kuvunja moyo sana.

Majibu ya Naibu Waziri huyo kwamba ati tayari gharama za umeme zilizopo nchini Tanzania ni hafifu ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki kutokana na serikali kuweka ruzuku kwa watumiaji, na ati kwamba bei iliyopo tayari serikali imeingiza ruzuku.

Sisi Hizb ut Tahrir Tanzania tungependa kutamka yafuatayo:

- Chini ya mfumo wa kibepari miradi hususan mikubwa kama Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere kamwe haipo kuhudumia ustawi wa raia, bali ipo kwa maslahi ya mabepari na wanasiwa waroho, bila ya kuwa na hisia yoyote ya kuwajali wananchi. Miradi hiyo na mfano wake imepachikwa jina na kuitwa 'miradi ya kimkakati' ikisemwa kwamba lengo lake ni kuja kusaidia raia. Tahamaki mambo yapo kinyume kabisa (haisaidii)
- Ni jambo la aibu sana kwa wanasiwa wa nidhamu ya kidemokrasia ya ubepari namna wanavyocheza 'tiki taka' za kisiasa (kufanya ujanja) katika mambo nyeti, wanasiwa hao hutoa kauli za kisanii kwa dhamira ya kubeza maslahi ya Umma. Siasa katika demokrasia sio suala la kuwatumiwa raia na kuchunga mambo yao kiuadilifu, bali siasa kwao ni fani ya kujikusanya utajiri haraka haraka ikiambatana na kauli za kisanii.
- Katika Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah hali iko tofauti kabisa na ubepari, umeme na mitambo (mikubwa) yote inayozalisha umeme na mfano wake ni mali ya Umma na hairuhusiwi kubinafsishwa, kutaifishwa au kufanya mali ya serikali.

Kwa hivyo, umeme hupaswa kusambazwa kwa watu wote na jitihada lazima ifanywe ya kupatikana umeme wa kutosha, tena kwa bei rahisi, (kama sio bure) na kamwe hausambazwi umeme kwa msingi wa kibiareshara.

Masoud Msellem

Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari

Hizb ut Tahrir Tanzania